


# Yale unahitaji kujua Kuhusu Kifua Kikuu

Kifua Kikuu (TB) ni ugonjwa unaosababishwa na vimelea ambavyo husambazwa kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mwingine kupitia kwa hewa. TB kwa kawaida huathiri mapafu, lakini pia inaweza kuathiri sehemu nyingine za mwili, kama vile ubongo, figo, au uti wa mgongo.

Si kila mtu aliyeambukizwa na vimelea vya TB hupata kuwa mgonjwa. Matokeo yake, huwa kuna hali mbili zinazohusiana na TB: maambukizo ya TB iliyolala (au TB isiyofanya kazi) na ugonjwa wa TB. Ikiwa hautatibiwa vizuri, ugonjwa wa TB unaweza kusababisha kifo.



## Tofauti Kati ya TB isiyofanya kazi na TB Inayofanya kazi


### Mtu aliye na TB Isiyofanya kazi

- Yuko na idadi ndogo ya vimelea vya TB katika mwili wake ambavyo viko hai lakini havifanyi kazi.
- Hana dalili na hajihisi mgonjwa.
- Hawezi kusambaza vimelea vya TB kwa wengine.
- Kwa kawaida ako na TB kwenye kipimo chake cha damu au maambukizi katika kipimo cha TB cha ngozi.
- Ako na x-ray ya kawaida ya kifua na kipimo hasi cha kohozi.
- Anahitaji matibabu kwa ajili ya TB isiyofanya kazi ili kuzuia ugonjwa wa TB.

### Mtu aliye na TB inayofanya kazi

- Ako na idadi kubwa ya vimelea vya TB vinavyofanya kazi mwilini mwake.
- Yuko na dalili na najihisi mgonjwa.
- Anaweza kusambaza vimelea vya TB kwa watu wengine.
- Kwa kawaida ako na TB kwenye kipimo chake cha damu au maambukizi katika kipimo cha TB cha ngozi.
- Anaweza kuwa na x-ray ya kifua isiyo ya kawaida, au kipimo chanya cha kohozi au vimelea vya kukuzwa.
- Anahitaji matibabu kwa ajili ya ugonjwa halisi wa TB.

**Ikiwa mwili wako hauwezi kuzuia vimelea vya TB visiendeleo kukua, huwa unapatwa na ugonjwa halisi wa TB. Dalili za TB halisi zinajumuisha:**



U.S. Department of Health and Human Services  
Centers for Disease Control and Prevention

## Kupima TB



Kupimwa na kutibiwa TB kunaweza kukuinga mwenyewe, familia yako na marafiki, na jumuiya yako. Kuna aina mbili za vipimo vya maambukizi ya TB: **Kipimo cha damu cha TB** na **Kipimo cha ngozi cha TB**.

### + Kipimo Chanya cha Maambukizi ya TB

Uko na vimelea vya TB mwilini mwako. Daktari atafanya vipimo vingine ili kubaini ikiwa uko na TB iliyolala au Ugonjwa wa TB halisi. Kipimo hiki kinaweza kujumuisha x-ray ya kifua, na kipimo cha kohozi unalokhoa.

### - Kipimo Hasi cha Maambukizi ya TB

Kipimo hasi inamaanisha pengine kuna uwezekano huna TB isiyofanya kazi au ugonjwa wa halisi wa TB.

#### Daktari wako anaweza kufanya vipimo zaidi ikiwa:

- Uko na dalili za ugonjwa halisi wa TB, kama vile kukohoa, maumivu ya kifua, joto kali, kupoteza uzito, au uchovu.
- Uko na maambukizi ya VVU.
- Kutangamana kwako na vimelea vya TB kulikuwa kwa hivi majuzi.


## Mwambie Daktari Wako ikiwa Ulipokea Chanjo ya TB

Vipimo vya damu vya TB ndicho kipimo kinachopendelewa kwa watu ambao wamepokea chanjo ya TB ya bacille Calmette-Guérin (BCG). Tofauti na kipimo cha ngozi cha TB, vipimo vya damu vya TB haviathiriwi na chanjo ya BCG.

Watu wengi waliozaliwa nje ya Marekani wamepokea ile chanjo ya TB ya BCG. Chanjo ya BCG haiwazuilii watu kikamilifu wasipatwe na TB. Mwachiriko chanya kwa kipimo cha ngozi unaweza kuwa ni kwa sababu ya chanjo ya BCG yenyewe au kutokana na maambukizi ya vimelea vya TB.



## TB Inaweza Kutibiwa



Vimelea vya TB vinaweza kuishi ndani ya mwili wako kwa miaka pasipo kusababisha dalili. Ikiwa uko na TB iliyolala, kuitibu ndiyo njia bora zaidi kujikinga usipatwe na ugonjwa halisi wa TB.

Ikiwa umepimwa ukapatikana kuwa na ugonjwa wa TB halisi, unaweza kutibiwa kwa dawa. Utahitaji kutumia na kumaliza dawa zako zote za TB kama ilivyoelekezwa na daktari wako au muuguzi. Hii ni kwa ajili ya kukufanya kujihisi vyema zaidi na kuzuia watu wengine wasipatwe na ugonjwa.

Njia bora zaidi ya kukumbuka kutumia dawa zako kwa ajili ya ugonjwa halisi wa TB ni kwa kupokea matibabu yanayoangaliwa moja kwa moja (directly observed therapy - DOT). Kupitia kwa DOT, utakutana na mhudumu wa uuguzi wa kiafya kila siku au mara kadhaa kwa wiki ama ana kwa ana au mtandaoni. Huyu mhudumu wa uuguzi wa kiafya atahakikisha kwamba zile dawa za TB zinafanya kazi jinsi zinavyofaa.